




Hapo zamani za kale, watu hawakujua chochote. Hawakujua kupanda mimea, kushona nguo, wala kuuunda vyombo vya chuma.

Lakini mungu aliyeitwa Nyame akiwa mbinguni, alimiliki hekima ambayo watu walihitaji. Nyame alihifadhi hekima hiyo kwenye chungu cha udongo.



Siku moja, Nyame aliamua kumpa Anansi chungu hicho kilichojaa ujuzi na hekima. Anansi alikitazama chungu kile. Na kila alipokitazama alipata kujua jambo jipya. Alifuarahi sana.



Anansi alisema moyoni,
"Nitakificha chungu hiki juu
ya mti mrefu ili mtu
mwingine asikifikie.
Ningetaka kufaidika peke
yangu." Kwa kutumia miyaa,
Anansi alitengeneza kamba
akaifungia kwenye chungu.

Kisha, alijifungia kamba hiyo
kiunoni. Aliupanda mti ule
huku kile chungu
kikining'inia mbele yake.
Haikuwa rahisi kwani kila
wakati, chungu kile
kilimgonga magotini.



Wakati huo wote, mwanawe Anansi alikuwa amesimama chini ya ule mti akimtazama babake. Hatimaye, alimwambia, "Baba, mbona usikifunge chungu mgongoni ili uweze kuuparaga mti?" Anansi aliamua kukifunga mgongoni chungu hicho kilichojaa hekima. Ilikuwa rahisi zaidi kukibeba kile chungu mgongoni.



Baada ya muda mfupi, alifika juu ya mti. Akiwa juu aliwaza, "Mimi ndiye ninabeba hekima lakini, mwanangu anaonekana kuwa mwerevu kuniliko." Anansi alikasirika na kukitupa kile chungu chini.



Chungu kilianguka na kuvunjika vigae vingi. Watu waliipata hekima wakajua kulima, kushona nguo, na kuunda vyombo vya chuma. Hivyo ndivyo watu walivyojua kufanya mambo yote wanayofanya.

